JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
**OFISI YA RAIS - MIPANGO NA UWEKEZAJI**
KITUO CHA UWEKEZAJI TANZANIA (TIC)

*Unapojibu tafadhali taja :*

**Kumb. Na.CA.148/234/01H/166** **07 Novemba, 2024**

Mkurugenzi,
Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni,
S.L.P 36009,
**KIGAMBONI**

YAH; **KUOMBA UTHIBITISHO WA UMILIKI WA ENEO LENYE UKUBWA WA EKARI 40.614 (MITA ZA MRABA 164,365) ENEO LA KIGOGO KISARAWE II-KIGAMBONI MANISPAA**

Kichwa cha habari hapo juu chahusika.

2 Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kimepokea maombi kutoka kwa kampuni ya **LOONG & ELEPHANT (TANZANIA) COMPANY LIMITED** ya kusajili mradi wa usafirishaji na Godauni *(transportation and warehousing)* na kupata cheti cha vivutio vya uwekezaji (*certificate of incentives).* Kampuni hiyo imeambatanisha mkataba wa mauziano ya viwanja hivyo baina yake na Kampuni ya **FHAAM LOGISTICS COMPANY LIMITED.**

3. Ili kuwezesha TIC kuendelea na taratibu za kusajili mradi wa Usafirishaji na Godauni tunaomba ofisi yako itoe uthibitisho wa umiliki pamoja na matumizi ya ardhi ya eneo tajwa lililopo Kigogo Kisarawe II Kigamboni Manispaa. Kufuatia umuhimu wa uwekezaji huu Katika Manispaa yako na rejea Kifungu cha 18 (4) cha Sheria ya Uwekezaji, 2022 kinachoitaka TIC kutoa mrejesho kwa wawekezaji ndani ya siku saba (7) ni matumaini yetu kwamba ombi hili litajibiwa kwa wakati.

4. Nashukuru kwa ushirikiano.

G.N. Mmassy
**Kny: MKURUGENZI MTENDAJI**

Nakala: Mkurugenzi,
Loong & Elephant (T) Co. Ltd,
S.L.P,
**DAR ES SALAAM**

Serikali za Mitaa, Sauti ya Wananchi,
Jitokeze Kushiriki Uchaguzi



CamScanner